

SHUKRANI KWA MUNGU WETU NDILO TENDO AMBALO
LINATIBUA KABISA MOYO WAKE KWA MHUSIKA
MAANDIKO: MWANZO 8:15-22

1. UTANGULIZI

Neno la shukrani linaweza kutafisiriwa na maneno mbali mbali, lakini yote jumla yake yanamezwa na neno moja tu kubwa la kusema **ASANTE!!** Kama ambavyo Mungu amefanya vitu vyake vyote muhimu kwa mwanadamu visiwe ghali sana maana watu maskini wasingeweza kumudu gharama zake (kama **usingizi hewa, maji, uzima,n.k** ndivyo binadamu yeyote aliye na afya njema kiakili na hasa baada ya kuokoka lazima ajae neno la shukrani kutoka ndani ya moyo wake kutokana na kutambua utendaji wa Mungu katika maisha yake kila wakati; na wakati wake wote atakiri kama mwandishi wa **Zab.124:1-8** alivyotambua na kukiri mara kwa mara kwamba “**kama siyo Bwana aliyekuwa pamoja na wao.....**

2. Kama kuna dhambi mbaya ambayo iliwagharimu sana wana wa Israel na kuwafanya wafe wengi jangwani, ni dhambi ya kutomkumbuka Mungu aliyewatoa mikononi mwa Farao kwa mkono wake hodari na akawaonya sana baadaye wasisahau kwamba bila Mungu akili zao na nguvu zao siyo chochote kabisa. **Kumb. 8:1-20.**

- **Ndugu zangu ni Yesu Kristo pekee ambaye ameongeza thamani ya maisha yetu ndiye ambaye ametutoa chini na kutuweka sasa hapa tulipo, ndiye ambaye ametuweka salama wakati rundo la wanadamu wengine wanaangamia; ndiye ambaye ametuponya wengi na magonjwa ambayo wengine wamekosa tiba yake; ndiye ambaye amelifanya hata Taifa letu la Tanzania kuwa tulivu na amani tele wakati wote n.k. Mekanisa hayajawahi kufungwa kwa hofu ya Covid 19; ukame haupo Tanzania wala tauni wala nzige wala watu kubaguana kwa ukabila au ukanda n.k**

3. Leo ndiyo sababu nimeupa ujumbe wangu kichwa kinachosema
“**shukrani kwa Mungu wetu ndilo tendo ambalo linatibua kabisa moyo wake na kumfanya atende zaidi na zaidi mambo makuu kwa yule aliyemshukuru kwa moyo wa dhati kabisa. 1 Samwl. 2:18-21(2:1-8)**

- **Mwanamke Hana na Mumewe Elikana** pamoja na mwanamke Mariamu wa **Luk. 1:26-38, 39-55** kwa kutambua kwamba mambo aliyowatendea Mungu yalikuwa juu ya uwezo wao **kuyapata**, walijaa mioyo ya shukrani mno jambo ambalo lilimfanya Mungu awabariki sana sana!!
- Ndugu yetu Nuhu baada ya kuokolewa yeye na familia yake tu, **Mwanz. 8:15-22**, alijenga madhabahu na kutoa dhabihu za shukrani. Tendo hili la Nuhu la kumshukuru Mungu ndilo lililoimarisha sana **uhusiano wake na Mungu kiasi cha Mungu kufanya Agano naye la kutoangamiza Ulimwengu tena!! Mwanzoni Mungu alimwambia atoke ndani ya safina na watoto wake akanyamaza**
- **Moyo wa shukrani wa kukaa chini na kukumbuka Mungu alikomtoa Mfalme Daudi ndiyo uliotibua mno moyo wa Mungu kiasi cha Mungu kutamka baraka ambazo hakuwahi kuzitamka kwa Mfalme yeyote kabla yake na baada yake. 2Saml. 7:1-16 (1Nyak. 29:1-6)**
- **Ibrahimu** sadaka yake ya shukrani kwa Mungu ikamfanya Mungu awe **rafiki** yake (washibane), asimfiche lolote analotaka kulifanya, ambariki na kuwa Baba yetu wa Imani kiroho hadi leo!! **Mwanz. 18:16-23, 22:13-19** (Jehova Yire) alama
- **Gideoni** alipoinuliwa na Bwana kutoka chini kabisa na kutoka katika ukoo duni mno; la kwanza Gideoni alimtolea sadaka ya shukrani na kujenga madhabahu kama ukumbusho. **Waam. 6:11-24**

“Yehova shalom” Moyo wa Mungu ukatibuka na kumtendea mambo makubwa mno.

4. **Asiwepo kati yetu ambaye Yesu Kristo atamshangaa leo kama alivyowashangaa Wayahudi hawa tisa ambao hawakuwa na moyo wa shukrani hata chembe ingawa Yesu aliwaponya ugonjwa mbaya wa ukoma. *Luk.17:11-19*. Maana kukosa moyo wa shukrani kunahashiria moyo wa kiburi ndani yako pamoja na mazoea ya kuzoelea baraka za Mungu na muda siyo mrefu kwa vyovyote vile utamwasi Bwana na utaishia pabaya kama lucifa naye alivyoasi na kutupwa kutoka Mbinguni.**

Ufun. 12:7-12

Ni neno jema kumshukuru Mungu!! ***Zab.92:1-6*** (yaani kumshukuru Mungu ni Neno ambalo **linamgusa** sana Mungu na **kuutibua** moyo wake zaidi kwa mhusika na kumbariki zaidi.

Mungu awabariki.

Na

Askofu Dr.L.M.Mwizarubi

Katibu Mkuu